

Buku la 7

BUKU LA 7

Salamu kwa familia ya Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb,

Mwanzo wa mwaka mpya wa masomo huwa wakati wa kufurahisha kila wakati, ijapokuwa mwaka huu utakuwa tofauti. Ninafuraha kwamba masomo ya mtandaoni yanaendelea na ninatazamia kuanza mwaka mpya wa masomo kwa upande sahihi. Tuna ujasiri kwamba upangaji wetu wa bidii na kujitolea kwa ufanisi kutatoa uzoefu bora kadri iwezekanavyo ya masomo ya mbali kwa wanafunzi wetu.

Ijapokuwa tulikumbana na changamoto chache wiki hii, wafanyakazi wetu waliweza kutatua masuala mengi kati ya hizi kuanzia muunganisho wa intaneti hadi usajili. Kila changanoto ni fursa ya kufanya vyema. Shukrani maalum kwa familia ambazo zilirudisha vifaa ambavyo havikutumiwa kwa sababu hii iliruhusu Idara ya Teknolojia ya Maelezo kusaidia wanafunzi wetu walio na mahitaji. Hivyo ndivyo inavyopaswa DCSD!

Wiki hii ningependa kusheherekea vipawa na talanta za ajabu za wanafunzi na wafanyakazi wetu. Bw. Mark Knowles kutoka kwa Early Learning Center aliwahimiza wanafunzi na somo la Bitmoji. Mzazi wa mwanafunzi mwenye umri wa miaka mitatu, Corinne alisema, “Bw. Knowles ni wa AJABU!!! Corinne hufurahia sana mazoezi ya kuchora na hasa kuchora picha binafsi ya Bw. Knowles. Utangulizi wake wa kuweza kuelewa jinsi anavyojielewa katika kuchora ni wa thamani. Anapenda pia ujumuishaji wake wa muziki na hadithi ili kuboresha somo.

Asante kwa kazi yako ya ajabu ya sanaa Bi. Corinne. Nimependezwa!

AFYA YA AKILI

Tunafuatilia visa vya COVID-19 na mpango wetu wa kushughulikia kufungua shule tena. Tunapoanza mwaka huu wa masomo, tunakumbushwa kwamba janga la COVID-19 limekuwa na kiwewe ambacho kinaathiri watoto wanaoenda shule na familia zao kwa njia tusizozitarajia. Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb ina mpango wa kushughulikia masuala ya kihisia, kisaikolojia, na maslahi ya kijamii kwa wanafunzi wetu. Mwanabunge wa Marekani Lucy Bath aliwasiliana na wilaya ya shule ili kupata maelezo kutoka kwa Idara ya Huduma za Kisaikolojia kuhusiana na msaada wa kihisia na kisaikolojia ambao wanafunzi na familia watapokea katika wilaya yake ya bunge. Mnamo Agosti 18, 2020, mwanasaikolojia wa shule Alanna Works, alihudumu kama mwanajopo mtaalamu alipowasilisha mada kuhusu “COVID-19 na Afya ya Akili.” Maonyesho na majadiliano ya Bi. Works yalitoa maelezo kuhusu takwimu za afya ya akili kwa wanafunzi wanaoenda shule, madhara ya kisaikolojia ya karantini katika watoto, na mapendekezo ya jumla ya kutoa msaada. Tungependa kutoa shukrani kwa Bi. Alanna Works, kwa kushiriki ufahamu wake wa kuhakikisha kwamba misaada inayofaa imewekwa kwa ajili ya wanafunzi, wafanyakazi, na familia.

Tunapoingia katika mwaka mpya wa masomo, maadili yetu yanasalia sehemu muhimu ya yale tunayofanya kama watumishi wa umma. Wakati wa mkutano wa mwisho wa Bodi, maelezo kuhusu Mpango Kamili Mkuu haukapatikana kabla ya mkutano huu. Uwazi ni sehemu muhimu ya kazi yetu katika elimu ya umma. Tafadhali rejelea hati hizi kwenye [Comprehensive Master Plan](#).

Nikifunga, ninashukuru sana wafanyakazi wetu wanaofanya kazi kwa bidii kuhakikisha wilaya yetu inafanya kazi kwa kiwango chake cha juu. Asante kwa wanafunzi na familia zetu ambao ni wavumilivu zaidi na sisi tunapokuwa tukisoma kwa mtandaoni kwa njia na mazingira mapya. Kuweni na wikendi njema!

Shabiki wenu #1,

Bi. Cheryl Watson-Harris, Msimamizi